MEI 2018

Wezesha Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki ili Tanzania ifikie Malengo ya Maendeleo Endelevu

UJUMBE MUHIMU

- Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki unaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu – kwa kuhakikisha kuwa huduma zinazotokana na mazingira zinaendelea kupatikana pamoja na kuwezesha jamii zinazotegemea misitu kufanya shughuli mbadala za kujikimu.
- Uwekezaji katika Milima ya Tao la Mashariki waweza kuwa ni mkakati wa kufikia malengo ya moja-kwa-moja na yale yasiyo ya moja-kwa-moja ya Maendeleo Endelevu na kuleta matokeo mbalimbali kwenye mazingira na kwa jamii.

Utangulizi na maelezo kwa ufupi

Kukamilika kwa kipindi cha utekelezaji wa Malengo ya Milenia kuliibua ajenda mpya ya maendeleo – Ajenda ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030 , iliyoamuliwa na wakuu wa nchi na serikali na wawakilishi wa ngazi za juu huko Marekani, katika Ofisi kuu za Umoja wa Mataifa zilizoko New York. Maamuzi hayo yalifanyika wakati wa Kongamano la Maendeleo Endelevu la tarehe 25-27, mwezi Septemba 2015. Ajenda hiyo ilijumuisha malengo 17 – yanayoitwa Malengo ya Maendeleo Endelevu na shabaha 169 ili kutokomeza umasikini, kupinga ubaguzi wa aina zote, kuleta haki, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ifikapo mwaka 2030. Kuanza kwa utekelezaji rasmi wa Malengo haya mapya pamoja na shabaha zake kulikubalika kuwa iwe ni tarehe 01/Januari 2016. Malengo haya yana sifa ya kuwa jumuishi na yasiyoweza kutenganishwa, na yenye sura tatu linganifu za maendeleo endelevu – yaani kiuchumi, kijamii na kimazingira. Kwa kuwa Malengo haya ni ya kidunia na yanayofaa kufikiwa kila mahala kwa ujumla wake, kila serikali (na Tanzania ikiwa ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa) ilipaswa kujipangia shabaha zake kulingana na mazingira halisi na vipaumbele vya nchi husika, lakini kwa kujumuisha Malengo hayo katika mfumo wa kitaifa wa mipango, katika ngazi za sera na mikakati huku zikihakikisha kuwa 'hakuna mtu atakayeachwa nyuma'. Nchini Tanzania, kwa mfano, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano tayari umejumuisha baadhi ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kama vile Lengo nambari 1, 2, 3, 4, 5, 7, 9 na 17.

Andiko hili linaelezea ni kwa namna gani mradi wa uhifadhi wa misitu unavyoweza kuwa na mchango mkubwa katika jitihada za kitaifa za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na shabaha zake. Andiko linaonyesha ni kwa namna gani uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki – kupitia ruzuku iliyotolewa kuwezesha miradi 204 ilivyoleta matokeo makubwa yanayoweza kuchangia katika Malengo ya Maendeleo Endelevu. Taasisi ya Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki – yaani Eastern Arc Mountains Conservation Endownment Fund (EAMCEF) ilipata ruzuku kutoka katika serikali ya Norway ili kutekeleza mradi wa miaka mitano (2011-2016) uliokuwa na lengo la kuhakikisha uhifadhi madhubuti na matokeo endelevu kwa ajili ya mfumo wa kiikolojia wa eneo la Milima ya Tao la Mashariki pamoja na kuboresha hali za maisha ya jamii zilizoko pembezoni mwa maeneo hayo. Ili kutekeleza mradi huu, EAMCEF ilitoa na kusimamia ruzuku kwa mamlaka za Halmashauri za Wilaya 11 zilizopewa kipaumbele, na maeneo tisa ya misitu ndani ya eneo la kiikolojia la Milima ya Tao la Mashariki. Miradi iliyotekelezwa katika maeneo ya hifadhi (maeneo 8 yakiwa ni Misitu ya Hifadhi za Asili na eneo moja ni Hifadhi ya Taifa) ilikuwa na lengo la kuboresha huduma za kiikolojia zinazotolewa na maeneo ya hifadhi pamoja na kuimarisha uwezo wa mamlaka zinazowajibika kusimamia maeneo husika – katika kundi hili ilitekelezwa miradi 40. Miradi ya uhifadhi na maendeleo ya jamii ilikuwa na lengo la kuboresha hali za maisha na ustawi wa jamii za pembezoni mwa hifadhi kwa kutekeleza miradi 146. Kundi la tatu la miradi lilihusu tafiti za bioanuwai na mabadiliko ya tabianchi.

Uhusiano wa mradi wa EAMCEF na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mradi wa miaka mitano (2011-2016) uliotekelezwa na Taasisi ya EAMCEF ulizaa matokeo mazuri yaliyoshawishi kukubalika kwa awamu ya pili ya ufadhili wa mradi, yaani 2016-2019 kwa bajeti ya Dola za Kimarekani Milioni 3.125. Matokeo ya awamu ya kwanza ya mradi huu yanaweza kuhusianishwa na pia kuchangia katika kufikia shabaha za Malengo ya Maendeleo Endelevu ndani ya ikolojia ya Milima ya Tao la Mashariki na katika ngazi ya taifa, hasa hasa katika mifano ya Malengo ya Maendeleo Endelevu nambari 1, 2, 5, 6, 7, 13, and 15.

Lengo Namba 1 – Kutokomeza Umasikini, likilinganishwa na mradi wa EAMCEF

SHABAHA HUSIKA

- Tokomeza umasikini uliokithiri kwa watu wote, mahali popote ifikapo mwaka 2030, kwa sasa umasikini uliokithiri unapimwa kwa watu wanaoishi kwa gharama ya chini ya Dola 1.25 za Kimarekani kwa siku.
- Punguza kiasi cha wanaume, wanawake na watoto wa umri wowote wanaoishi katika umasikini wa aina mbalimbali katika nchi husika angalau kwa nusu ifikapo mwaka 2030
- Hakikisha kuwa wanaume na wanawake wote, na hasa hasa walio masikini na walio katika mazingira hatarishi, wanakuwa na haki sawa za rasilimali za kiuchumi...umiliki wa ardhi, maliasili, teknolojia mpya inayofaa... ifikapo mwaka 2030.

Mradi wa EAMCEF – Uhusiano na Mchango wake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

- Kazi kuu ya mradi wa Taasisi ya EAMCEF si tu kuhifadhi mfumo wa ikolojia wa milima, lakini ni kuboresha pia hali za maisha za jamii zilizoko pembezoni kwa kuwezesha ufanyaji wa shughuli mbadala za kujipatia kipato.
- EAMCEF ilitoa ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya jamii ya uhifadhi na maendeleo iliyolenga katika kuboresha hali za maisha na ustawi wa jamii zilizoko pembezoni mwa hifadhi za misitu.
- Kupitia shughuli mbadala za kujipatia kipato, jamii zimefanikiwa kuongeza kipato chao cha kaya, kuboresha hali za maisha, kuongeza mara mbili uzalishaji katika mazao ya chakula na hivyo kuchangia katika kupunguza hali ya umasikini.
- Pia, wanavijiji waliojipatia kipato kutokana na ajira za muda mfupi katika shughuli za uhifadhi wa misitu wameweza kujiongezea kipato binafsi.
- Mradi wa EAMCEF ulihamasisha ushiriki wa wanawake na wanaume wa umri mbalimbali - wakiwamo vijana na watu walioko katika mazingira magumu. Vilevile, sambamba na shughuli za upangaji wa ardhi, mradi uliwezesha utolewaji wa hati za kimila la umiliki wa ardhi kwa zaidi ya wanavijiji 1,650 na hivyo kuimarisha na kuhakikisha usalama wa haki za umiliki wa ardhi na rasilimali zake.

Lengo namba 2 – Kukomesha njaa, likilinganishwa na mradi wa EAMCEF

SHABAHA HUSIKA

- Ondoa njaa na hakikisha kuwa watu wote, na hasa hasa masikini na watu waliopo kwenye mazingira hatarishi, wakiwamo watoto wadogo – wanapata chakula salama, chenye lishe bora na cha kutosha ifikapo mwaka 2030.
- Ongeza mara mbili uzalishaji katika kilimo na kipato cha wakulima wadogo wadogo, na hasa hasa wanawake, watu wanaoishi maisha ya asili, familia za wakulima, wafugaji na wavuvi, ikiwamo kwa kupitiaupatikanaji wa uhakika wa... ajira zisizo za mashambani ifikapo mwaka 2030.
- Hakikisha uwepo wa mfumo endelevu wa uzalishaji chakula na tekeleza shughuli stahimilivu za kilimo zinazoongeza uzalishaji na mavuno, zinazolinda uwezo wa mfumo wa ikolojia katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi, majanga ya hali ya hewa...na zinazoimarisha ubora wa ardhi na rutuba yake ifikapo mwaka 2030.

Mradi wa EAMCEF – Uhusiano na Mchango wake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

- Shughuli za mradi, na hasahasa kupitia uanzishwaji wa kilimo hifadhi, zimesababisha ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula kutokana na uhifadhi wa maji na udongo – hivyo, kuhakiksha upatikanaji wa chakula kwa kipindi cha mwaka mzima.
- Shughuli nyingine za kilimo zilizofadhiliwa na mradi – kama vile, mbegu zilizoboreshwa, kilimo cha alizeti, maharage ya soya, ufugaji wa samaki, na upandaji miti – zimesaidia kuongeza kipato cha wakulima wadogo, na kuleta manufaa mengine mbalimbali.
- Uanzishwaji wa shughuli za ufugaji wa kuku wa kienyeji walioboreshwa na ufugaji wa mifugo umekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha lishe.
- Fursa za ajira nje ya zile za kilimo, kama vile ushiriki wa wanajamii katika shughuli za utalii na usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi (kama vile usafishaji wa mipaka, patroo, na uchimbaji wa mitaro) zimekuwa chanzo muhimu cha mapato ya msimu kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo.
- Uanzishwaji wa mbinu za kilimo hifadhi umekuwa chachu ya mabadiliko kwa jamii zinazoishi milimani na katika miteremko mikali ya Wilaya ya Muheza, Manispaa ya Morogoro na Wilaya ya Morogoro.
- Mradi ulitoa mafunzo kuhusu mbinu za uhifadhi wa udongo na maji kwa wanavijiji 329 (wanawake 139 na wanaume 190), mafunzo hayo yalisababisha jumla ya eneo lenye ukubwa wa ekari 863 kulimwa kisasa kwa mbinu hii, na hivyo kuongeza uzalishaji kufikia mara tatu zaidi.

Lengo namba 5 – Usawa wa Jinsia, likilinganishwa na mradi wa EAMCEF

SHABAHA HUSIKA

- Komesha aina zote za ubaguza, mahali popote, kwa wanawake na wasichana.
- Hakikisha ushiriki kamili na madhubuti wa wanawake na fursa sawia za uongozi katika ngazi zote na ufanyaji maamuzi katika siasa, uchumi na maisha ya umma.

Mradi wa EAMCEF – Uhusiano na Mchango wake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

- Kwa ujumla, utekelezaji wa miradi ya EAMCEF ulihakikisha ushiriki wa asilimia 48 ya wanawake, ikiwamo wasichana. Katika baadhi ya miradi, mradi ulisaidia vikundi vilivyoundwa na wanawake tu (100%), kama vile mradi wa ujenzi wa majiko bora, kilimo cha miti ya viungo na kilimo cha uyoga.

- Mradi wa EAMCEF ulisaidia pia watu wenye ulemavu na na wanaoishi na Virusi vya Ukimwi katika Wilaya ya Mufindi.
- Mradi uliwezesha ushiriki na mgawanyo wa manufaa katika utekelezaji wa miradi kwa watu wa umri mbalimbali, wakiwamo wanawake, wasichana na vikundi vilivyoko katika mazingira magumu.
- Mradi uliwezesha uanzishwaji na uendeshwaji wa Kamati za Ushauri 'Local Advisory Committees' katika kila Wilaya za mradi. Kamati hizi zilijumuisha wanasiasa (madiwani) na wataalamu, ikiwamo pia wawakilishi wa wanawake.
- Ajira za muda mfupi, zilizolenga kutoa fursa kwa jinsia zote, hasa hasa katika shughuli za usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi zilihakikisha uwiano wa wanaume na wanawake, Zaidi ya wanavijiji 3,500 walinufaika kutokana na fursa za ajira.

Lengo namba 6: Maji Salama na Usafi, likilinganishwa na mradi wa EAMCEF

SHABAHA HUSIKA

- Hakikisha watu wote wanapata na wanamudu gharama za maji ya kunywa yaliyo salama ifikapo 2030
- Linda/hifadhi na rejesha mifumo ya kiikolojia inayohusiana na maji, ikiwamo milima, misitu, maeneo oevu, mito, hifadhi za maji aridhini na maziwa ifikapo 2030.

Mradi wa EAMCEF – Uhusiano na Mchango wake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

- Misitu katika Milima ya Tao la Mashariki ni vyanzo vya maji ya mito mingi inayotegemewa na watu wengi katika nyanda za chini na katika maeneo ya jirani na ya mbali, ikiwamo jiji la Dar es salaam – kwa matumizi ya nyumbani na viwandani karibu asilimia 25 ya idadi kamili ya watu nchini walioko katika miji ya mikoa ifuatayo; Iringa, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma, Dar es salaam, na Pwani.
- Mito mikuu inayotegemea maji kutoka katika Milima ya Tao la Mashariki ni pamoja na; Mto Ruaha Mkuu, Kihansi, Pangani, Hale, Wami, Kilombero, Rufiji na Mto Ruvu.

Lengo namba 7 – Nishati Mbadala kwa gharama nafuu, likilinganishwa na mradi wa EAMCEF

SHABAHA HUSIKA

- Hakikisha upatikanaji wa huduma za nishati nafuu, ya uhakika na ya kisasa ifikapo mwaka 2030.
- Ongeza matumizi ya nishati jadidifu kwa kiasi kikubwa katika matumizi ya nishati ulimwenguni ifikapo 2030.
- Ongeza mara mbili kiwango cha kidunia cha uboreshaji wa ufanisi wa matumizi ya nishati ifikapo mwaka 2030.
- Panua miundombinu na kuza teknolojia kwa ajili ya usambazaji wa huduma za kisasa na endelevu za nishati kwa watu wote katika nchi zinazoendelea ifikapo 2030.

Mradi wa EAMCEF – Uhusiano na Mchango wake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

- Mradi uliwezesha huduma ya nishati ya kisasa kwa kuanzisha teknolojia ya nishati ya gesi itokanayo na viumbe hai (biogas) kwa ajili ya matumizi ya nyumbani – hivyo kusaidia kuokoa kiasi cha asilimia 50% cha matumizi ya kuni zilizokuwa zikivunwa katika misitu ya jirani. Mradi ulitoa mafunzo kwa wanavijiji 97 na mafundi 25 wa Wilaya ya Kilolo, Mkoa wa Iringa, pia mradi uliwezesha ujenzi wa mitambo 12 ya kuzalisha gesi katika kaya zilizochaguliwa.
- Kwa kuwa mabwawa mengi yanayotumika kuzalisha umeme yanategemea maji ambayo asili yake ni katika Milima ya Tao la Mashariki, uhifadhi wa misitu ulihakikisha kuwa maji yanaendelea kupatikana na hivyo kuwa na uhakika wa upatikanaji wa umeme.
- Asilimia tisini (90%) ya umeme unaotokana na maji unazalishwa katika mabwawa makuu ya Kidatu, Mtera, Kihansi, Nyumba ya Mungu, Pangani na Hale – ambayo yote yanapokea maji ambayo vyanzo vyake ni katika Milima ya Tao la Mashariki.
- Mradi ulianzisha majiko bora yanayotumia nishati vizuri pamoja na teknolojia ya gesi inayotokana na wanyama (biogas) ili kupunguza matumizi ya kuni.
- Mradi ulitoa mafunzo ya ujenzi wa majiko bora kwa wakufunzi 1,531. Mpaka kufikia mwisho wa mradi, jumla ya kaya 14, 016 zilishaanza kutumia majiko bora – na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya kuni kwa zaidi ya asilimia 50, hivyo kupunguza kasi ya uharibifu wa misitu.

Lengo namba 13: Hatua Dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi, likilinganishwa na miradi ya EAMCEF

SHABAHA HUSIKA

- Boresha elimu, kuza uelewa na uwezo wa watu na taasisi kuhusu kukabiliana, kuhimili kupunguza athari na tahadhari ya mapema juu ya mabadiliko ya tabianchi.

Mradi wa EAMCEF – Uhusiano na Mchango wake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

- Shughuli za kukuza uelewa katika mradi wa EAMCEF zilihusisha kutoa elimu ya uhifadhi, na masuala yanayohusiana na kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kilimo hifadhi, na upandaji miti.
- Mradi ulisaidia utekelezaji wa tafiti zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi na misitu – kiwango cha kaboni ya misitu, pamoja na viashiria vya mabadiliko ya tabianchi.

Lengo namba 15 – Kulinda Uhai katika Ardhi, likilinganishwa na mradi wa EAMCEF

SHABAHA HUSIKA

- Hakikisha uhifadhi, urejeshaji na matumizi endelevu ya mifumo ya kiikolojia na huduma zake iliyoko ardhini na katika maji, na hasa hasa misitu, maeneo oevu, milima na ardhi kavu... ifikapo 2020.
- Endeleza usimamizi endelevu wa aina zote za misitu, punguza kasi ya ufyekaji wa misitu, rejeleza misitu iliyoharibiwa na ongeza upandaji na urejeshaji wa misitu ulimwenguni ifikapo 2020.
- Hakikisha uhifadhi wa mifumo ya kiikolojia ya milima, ikiwamo bioanuwai zake ili kuendeleza uwezo wake wa kuleta manufaa yaliyo muhimu kwa maendeleo endelevu.
- Tekeleza jitihada za haraka na zenye tija ili kupunguza uharibifu wa mazingira asili, punguza upotevu wa bioanuwai, na mpaka kufikia 2020, linda na zuia upoteaji wa viumbe vilivyo hatarini.
- Wezesha mgawanyo sawia na linganifu wa faida zitokanazo na matumizi ya rasilimali za kijenetiki na wezesha upatikanaji wa rasilimali hizo, kama ilivyokubalika kimataifa.
- Tekeleza jitihada za haraka za kutokomeza ujangili na usafirishaji wa viumbe – Wanyama na mimea - vilivyolindwa na tokomeza uhitaji na usambazaji wa bidhaa haramu za viumbepori.

Mradi wa EAMCEF – Uhusiano na Mchango wake katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

- Lengo namba 15 ndilo kitovu cha mradi wa EAMCEF. Lengo la mradi ambalo ni 'kuwezesha uhifadhi wa misitu ya Milima ya Tao la Mashariki iliyoko upande wa Tanzania ambalo ni eneo pendekezwa la urithi wa dunia' linamaanisha utekelezaji wa shughuli kadhaa zinazoendana na shabaha (za Malengo ya Maendeleo Endelevu) namba 15.1, 15.2, 15.4, 15.5, 15.6, na 15.7. katika hili, mradi ulifanikiwa kufanya mambo yafuatayo:
- Kusaidia uandaaji wa mipango ya usimamizi wa misitu
- Urekebishaji wa mipaka ya misitu inayofikia jumla ya kilomita 1,500.
- Kuwezesha kurejea kwa eneo la mistu kupitia upandaji wa miti katika maeneo yaliyoharibiwa, udhibiti wa mioto-pori, kufukia maeneo ya machimbo yaliyochimbwa kinyume cha sheria ndani ya misitu.
- Mradi uliimarisha doria za misituni na kuwezesha kupungua kwa uvamizi wa maeneo ya misitu uliokuwa unatokana na shughuli za kilimo, uwindaji na uchimbaji wa madini.
- Jamii zinazoishi pembezoni mwa mistu ziligawiwa manufaa yaliyotokana na shughuli za utalii, pamoja na uuzwaji wa mazao na vifaa vilivyotaifishwa msituni. Jumla ya Tsh. 450,000,000 ziligawanywa kwa wanajamii.
- Zilitolewa ajira za muda mfupi na malipo kwa ushiriki katika doria za pamoja.
- Doria madhubuti za kukabiliana na shughuli haramu misituni, ikiwamo kufungua kesi mahakamani dhidi ya wahalifu.

Andiko hili limeandaliwa kutoka kwenye Ripoti ya Matokeo ya Mradi wa Kuboresha Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania 'Improving Conservation of the Eastern Arc Mountains of Tanzania' (2011-2016), kwa msaada kutoka Serikali ya Norway.

Kwa taarifa Zaidi, wasiliana na:
Sekretarieti ya Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki,
Kitalu Na. 348, Eneo la Forest Hill, Barabara ya Kingalu,
S.L.P 6053,
Morogoro, TANZANIA.

+255 23 293 4274 +255 755 330 558 +255 23 293 4273

eamcef@easternarc.or.tz | www.easternarc.or.tz